JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**



CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**


**Namba za Simu 0784903689**

**Mkuu wa Shule 0742305798**

**Makamu Mkuu wa Shule 0769048680**

**Patron 0746909392**

**Shule ya Sekondari SANYA JUU**

**S.L.P 84 SANYA JUU**


**Tarehe 12/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**

**..................................................**

**S.L.P ..........................................**

**..................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SANYA JUU HALMASHAURI YA SIHA MKOA KILIMANJARO MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ............

Shule ya Sekondari **SANYA JUU** ipo umbali wa Kilometa 50 Kaskazini-Magharibi mwa mji wa **MOSHI.** Usafiri wa basi kutoka mjini **MOSHI** unapatikana katika kituo cha mabasi MOSHI MJINI nauli ni shilingi za kitanzania 2000/=.

Ukitokea Arusha unashuka eneo linaitwa BOMANG'OMBE na kupanda magari ya SANYA JUU kwa nauli ya Tshs 1000/=. Shuka kituo kinaitwa SANYA DAY.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 14/8/2023. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/8/2023. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/8/2023

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Suruali nyeusi mbili zisizobana miguu (zisiwe model), ziwe na upana wa "inch17" kwenye miguu, mifuko mitatu isiyo na zipu,

ii. Mashati meupe mawili ya mikono mirefu yasiyo na urembo wowote na yasiyobana mwili.

iii. T-shirt ya shule (Itapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 15,000/=)

iv. Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.

v. Soksi jozi mbili nyeusi

vi. Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi isiyo na bakolu kubwa au zenye urembo.

vii. Sweta moja rangi ya bluu nyeusi (Dark blue) liwe na shingo ya V.

viii. Nguo za kushindia (shamba dress) ni truck suit rangi ya light blue na T-shirt ya rangi ya light blue isiyo na maandishi

ix. Tai moja rangi nyeusi,

x. Sare ya michezo kwa shule hii ni Bukta moja rangi ya bluu na T-

shirt moja rangi ya bluu (sare hizi zitavaliwa wakati wa michezo tu).

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari aje na counter 12 quare 4
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na godoro kutoka nyumbani. Godoro lisilopungua inch 2 1/2 x 6
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue, blanket 1, mto na foronya 2 zenye rangi ya blue, chandarua 1
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko
xi. Jembe jipya 1 na mpini wake, squeezer/mopa 1, brush ya chooni 1, hard broom 1 na dawa ya kusafishia chooni lita 1.

**2.3 Michango mbalimbali**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Taaluma | 20,000/= |
| 2. | Ukarabati | 15,000/= |
| 3. | Mpishi, Mlinzi na Patron | 30,000/= |
| 4. | Tahadhari | 5,000/= |
| 5. | Nembo | 5,000/= |
| 6. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha zote zilipwe kwenye Akaunti ya shule No. 40101200100. Katika Benki ya NMB. Jina la akaunti ni SANYA JUU SECONDARY SCHOOL**

**2.4 Matibabu / Afya**

Mwanafunzi ambaye ana Bima ya afya ya NHIF aje nayo shuleni pamoja na sh. 9,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza. Mwanafunzi asiye na Bima ya afya atatakiwa kuja na sh. 15,000/=, Yenye mchanganuo ufuatao:- sh. 6,000/= atakatiwa Bima ya afya ya CHF na sh. 9,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na



CamScanner

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;



CamScanner

xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SANYA JUU SECONDARY SCHOOL**

**Saini ya Mkuu wa Shule**.......................................

**Jina la Mkuu wa Shule . <u>BADI JAFARI MMBAGA</u>**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ........................ MKUU WA SHULE SANYA JUU SEKONDARI S.L.P 84 SANYA JUU

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule …0784903689/0742305798.
- Makamu Mkuu wa Shule 0769048680
- Mwandamizi Taaluma 0762891186
- Mwandamizi Malezi 0746909392



CamScanner

## TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

**Mimi (mwanafunzi)......................................................................... umri.........**
**Jina la (Mzazi)................................................................................ umri........**
**Kata........................Tarafa..............................Wilaya...................................**
**Namba ya simu............................................ S.L.P...........................................**

**Nani anakulipia michango (mzazi/mlezi)..........................................umri.....**
**Kata........................Tarafa.........................................Wilaya...........................**
**Namba ya simu............................................ S.L.P...........................................**

**Kiri kama utafuata sheria za shule (mwanafunzi)**
**.......................................................................................................................**
**.......................................................................................................................**
**.......................................................................................................................**
**.......................................................................................................................**
**Kiri kama utakamilisha ulipaji wa michango ya shule (mzazi/mlezi)**
**.......................................................................................................................**
**.......................................................................................................................**
**...........................................................................................**
**Jina la mwanafunzi……..............................sahini............ tarehe...........**
**Jina la (mzazi/mlezi)..............................................sahini...............tarehe.......**

**NB:Mwanao anapaswa kujaza fomu ya matibabu iliyoambatishwa na maelezo haya na kuiwasilisha shuleni siku hiyo ya kuwasili.**



CamScanner

# ORODHA YA VITABU:

Kutokana na uhaba wa vitabu, mzazi/mlezi anashauriwa kumnunulia mwanae vitabu vitakavyomsaidia katika rejea na mazoezi mengine kulingana na mchepuo anaosoma kwani vitabu vilivyopo havitoshelezi kila mwanafunzi kupata kitabu chake mwenyewe. Baadhi ya vitabu hivyo ni kama vifuatavyo:-

**ADVANCED MATHEMATICS.**

1. Advanced mathematical TIE form 5&6
2. Advanced Level Pure Mathematics, Fourth Edition by C. J.Tranter
3. Pure Mathematics, by J.K Backhouse
4. Engineering Mathematics sixth edition by K. A.STROUD
5. Advanced Mathematics1-review (problems & solutions)
6. Advanced Mathematics 2-review (problems & solutions)

**BASIC APPLIED MATHEMATICS:**

1. Basic applied mathematics TIE form 5&6
2. Additional and Applied Mathematics by J. F.TALBERT
3. Basic applied mathematics (BAM) by Respicius Kiiza and Lugano Mwanginde
4. Basic applied mathematics review questions and solutions

**BIOLOGY**

1. Biology TIE form 5&6
2. Biological science by D.J.Taylor
3. Biology for form V&VI by Nyambari Nyangwine
4. Biology Questions and answers
5. Biology for Advanced level, new understanding, 4th Edition by Gleen & Susan Toole

**CHEMISTRY**

1. Chemistry TIE form 5&6
2. Chemistry in action (Michael Fremantro)
3. Advanced chemistry by Michael Clugston, Rosalind Flemming
4. Comprehensive approach to advanced level CHEMISTRY questions with answers by Sedrick C. Magas, & Kira Ernest

5. Advance chemistry-review
6. Physical chemistry with General chemistry (Advenced) by Mark Daniel Hermes Daniels.

**GEOGRAPHY**

1. Geography TIE form 5&6
2. Practical Geography by Zist Kamil
3. Approach to physical geography questions by Ahmed Lubwana
4. A comprehensive approach to physical geography for secondary school by Nyambari Nyangwine
5. Geography paper two by Msabila D.T. Msabila
6. An integrated Geography by Msabila
7. Physical geography by D.T.Msabila

**PHYSICS**

1. Physics TIE form 5&6
2. Advanced level physics 7th Edition by Nelkon and Parker
3. Advanced physics by Sterv Adams and Jonathan Allday
4. Advanced physics review
5. Principle of physics by Chand

**GENERALSTUDIES**

1. General study TIE
2. Contemporary Approach for advanced level general studies notes (form 5 & 6)



CamScanner

**PRESIDENT OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**SIHA DISTRICT COUNCIL**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**To be completed by a medical officer in respect of all form ones and five who join the school**

**P ART A: TO THE MEDICAL OFFICER**

**.................................................................................................**

**STUDENT FORM**
**NAME: .............................................................................................................**

**Please examine the above named person is to be admitted to secondary school education.**
**Signature.......................Designation.** HEAD OF SCHOOL**....Name of head of school...** BADI JAFARI MMBAGA **..........Official stamp...** HEADMASTER SANYA JUU SEC.SCHOOL P.O.BOX 84 SANYA JUU

**P ART B: TO BE COMPLETE BY MEDICAL OFFICER**
**Blood corny (red and white)...............................**
**Stool examination..........................................T.B. test.......................................**
**Eye test.........................................................Ears.......................................................**
**Chest..............................................................Spleen...........................................**
**Abdomen...................................Pregnancy (girls only).......................................**

**ADDITION INFORMATION (e.g. physical defeat or impairments)**

**.......................................................................................................................................**
**.......................................................................................................................................**

**Please certify that the above is fit to be admitted/ taken care in secondary school. Kind of care**

**.......................................................................................................................................**

**P ART C: M EDICAL OFFICER CERTIFICATE**

**I have examined the above named person and consider that *he/she* is not physically fit joining secondary education.**
**Doctor's name.....................................................................signature.........................**
**Station.................................... Date........................**

**.................................................**
**Official stamp**



CS CamScanner